OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII MAGAZETINI NA MITANDAONI

21/04/2025 ► 25/04/2025

OAG

The Guardian
www.ippmedia.com
ISSN 0856 - 5434 ISSUE No. 9461 • PRICE: Tsh 1,000, Kenya sh100
TANZANIA
THURSDAY 24 APRIL, 2025

National Pg 3
VP: Promote African cuisine to power tourism growth



National Pg 5
Streetlights credited with drop in criminal activities



National Pg 6
Court of Appeal judges trained on IP law and new technology



# Samia unveils new edition of refreshed laws costing 10bn/-

*The project was a direct outcome of changes within the Attorney General's Office, including expansion of its workforce and investment in internal legal capabilities*

By Guardian Reporter

THE newly launched 2023 revised edition of laws, costing a total of 10bn/-, underscores Tanzania's growing ability to independently manage complex national projects that once relied on foreign support, the government has affirmed.

President Samia Suluhu Hassan made this observation here yesterday at the launch of the revised edition, the most comprehensive update of Tanzania's legal framework since 2002, reaffirmed the government's strong commitment to legal reform and the strategic use of domestic resources to drive national development.

The president underscored the significance of homegrown solution to sharpen the nation's progress, while stressing the historic character of releasing new editions of the country's laws.

The exercise was successfully completed using government funding and implemented exclusively by local legal experts over a four-year period. "The completion of this legal revision marks a major milestone in our nation's governance journey," she stressed.

"It reflects our resolve to build internal capacity and pursue sustainable, homegrown solutions to national challenges," she specified, noting that issuing a new edition is aligned with the broader agenda of strengthening institu-

TURN TO PAGE 2




President Samia Suluhu Hassan signs three copies of laws that have been amended in accordance with section 17 of the Laws Revision Act at State House Chamwino in Dodoma yesterday. Photo: State House



# Samia unveils new edition of refreshed laws costing 10bn/-

FROM PAGE 1

tional independence, promoting good governance and enhancing transparency.

"This time, by relying entirely on our internal resources—both financial and human—we are demonstrating our national maturity and confidence in our own capabilities," she further noted.

The 2023 Revised Edition of Laws consolidates 446 principal legislations into 21 volumes and incorporates 171 new laws enacted between 2002 and 2023. The process involved harmonising overlapping legal texts, correcting editorial errors and updating outdated legal provisions to reflect Tanzania's current social and economic landscape, officials said.

The president underscored that a modern, coherent legal system is foundational to justice, public participation and economic progress. "A well-structured legal framework empowers citizens, promotes public trust, and is a key driver of national development," she emphasised.

She urged stakeholders to embrace and utilise the revised legal framework, asserting that legal reform is a testament to Tanzania's determination to build a just, modern and self-reliant nation.

The Attorney General's Office needs to complete the translation of Tanzanian laws into Kiswahili, including the new compendium of revised laws in its 2023 edition, she stated.

A system needs to be established to ensure easy public access to the updated laws—digitally and in print—to promote awareness and understanding of citizens' rights, she asserted.

"Laws reflect a nation's civility. Without clear laws, justice cannot prevail. If the law is not accessible, the protection of rights is uncertain, which undermines peace and hampers economic activity," she further noted.

Delays in publishing revised volumes of laws deny citizens their rights, as those responsible for decision-making may be unaware of newly enacted legislation. The availability of the 2023 Revised Edition will help remedy this by consolidating all 446 principal laws into a single, well-organised and easily accessible reference, the president noted.

Access to the revised edition will reduce the time courts spend researching legal precedents, enhance transparency, build public trust in the government, curb abuse of power by closing legal loopholes that enable corruption, and strengthen the rule of law, she stated.

In turn, this situation will elevate Tanzania's standing economically, politically and socially, she said, while Attorney General Hamza Johari, who presided over the revision process, hailed this achievement as a reflection of institutional growth.

"The project was a direct outcome of changes within the Attorney General's Office, including expansion of its workforce and investment in internal legal capabilities," he said.

"Unlike the 2002 revision funded by the World Bank, this exercise was entirely financed through government revenues," he said, noting that it represents a major shift towards self-reliance in managing our legal system.

The revised laws are set to come into force on July 1, serving as a vital reference for legal practitioners, the judiciary, government institutions, educators and the general public, he added.

# Tanzania yajiimarisha utoaji haki

Na Selemani Nzaro

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema sheria zilizofanyiwa urekebu Toleo la Mwaka 2023 litarahisisha upatikanaji wa haki na kuongeza kasi ya ukuaji uchumi.

Akizindua toleo hilo Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma jana, Rais Samia amesema bila sheria zinazoeleweka, zilizowekwa wazi na zinazoendana na wakati uliopo, haki haiwezi kutendeka.

Amesema bila sheria kuwa wazi uhakika wa ulinzi wa haki kwa watu unatoweka na kusababisha urasimu wa amani na kuongeza shaka katika biashara na uwekezaji.

Alisema urekebu wa sheria utarahisisha upatikanaji wa haki kwa wananchi kwa sababu sheria zote kuu 446 zimehuishwa katika mabadiliko hayo.

Kazi hiyo imefanywa na wataalamu wa ndani na kutumia Sh bilioni 10.

Rais Samia alisema urekebu wa sheria utapunguza muda unaotumiwa na mahakama katika kutafsiri sheria fulani inayohitajika kutumika katika kutoa uamuzi.

"Kutokuwepo kwa jumla zilizorekebishwa kwa wakati, kwa kiasi fulani kunachangia kunyima haki za watu kwa sababu wanaoamuliwa kutoa maamuzi wanakuwa hawako kwenye kupata uelewa wa marekebisho yaliyofanywa kwa wakati fulani," alisema Rais Samia.

Rais Samia alisema urekebu wa sheria hizo utajenga imani ya wananchi kwa serikali yao kwa sababu watapata haki kwa wakati.

Alisema kuziweka pamoja sheria zote ni nyenzo muhimu ya kupunguza matumizi mabaya ya madaraka na kuziba ombwe la kisheria lililokuwa likitumika kuchochea rushwa katika mchakato wa utoaji wa haki nchini.

Vilevile alisema kuweka pamoja kwa sheria hizo kutaongeza imani kwa wafanyabiashara na wawekezaji katika kutimarisha shughuli za kiuchumi nchini.

Rais Samia alisema kuandikwa kwa jumla hiyo ya sheria kutapunguza uwezo kuno wa wananchi kufanya makosa kwa kisingizio cha kutojua sheria.

"Urekebu wa sheria ni nyenzo muhimu ya kupunguza matumizi mabaya ya madaraka na kuziba ombwe la kisheria lililokuwa likitumika kuchochea rushwa hapa sasa linaenda kuzibwa, ile tasama haka tasama kule ili kupata ombwe la kupenyeza yake sasa hakuna," alisema Rais Samia.

Alieleza kuwa kazi ya urekebu wa sheria za nchi kuanzia mwaka 2003 hadi 2023 imepitia hatua ya changamoto za msingi kwenye tasnia ya sheria na kuongeza hadhi ya taifa kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Ameagiza Kampuni ya Awamu ya Pili ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia ibebe ajenda ya urekebu wa sheria ili ueleweke kwa wananchi na watumie katika kutafuta haki zao.

Aidha, amemwagiza Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali kuhakikisha jumla ya sheria zilizorekebishwa zinatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili iwe rahisi kwa wananchi kusoma na kuelewa.

Ametoa rai kwa mahakama itumie sheria hizo kama msingi wa utoaji wa haki nchini na akaagiza mawakili wa serikali, mawakili wa kujitegemea na maofisa sheria wawe mabalozi wa kuenezа uelewa wa sheria hizo.

Aidha, ameviomba vyombo vya habari vishirikiane na Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuelimisha wananchi kuhusu sheria hizo na umuhimu wake.

Alitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ihakikishe sheria hizo zinapatikana kirahisi kwa wananchi kwa maana ya kuzifikia kupitia mitandaoni ili wasome na kuzielewa.

"Sheria ni msingi wa haki, amani na maendeleo ndio maana serikali inajielekeza na kuwekeza katika fani ya sheria na kufanya yote yanayostahiwa kufanywa ndani ya fani ya sheria na mahakama ili kuweka msingi imara wa haki, amani na maendeleo kwa nchi yetu," alieleza Rais Samia.

Alisema kujatekeleza hayo ni lazima kwa sababu sheria ndicho kiini cha ustawi wa taifa na kwamba bila sheria zinazoeleweka na kuwekwa wazi itakuwa vigumu haki kupatikana.

Rais Samia alisema takwimu za marekebisho ya sheria kati ya mwaka 2003 hadi 2023 zinaonesha jumla ya marekebisho 1,039 yamefanyika.

Alisema serikali itaendelea kuwekeza katika mabadiliko ya sheria kwa kuendana na mahitaji yanayojitokeza na kwamba urekebu wa sheria utakuwa ukifanyika kila baada ya miaka 10 badala ya utaratibu uliopita wa miaka 20.

Alisema urekebu wa sheria utakaofuata utafanyika mwaka 2033 wakati wa Serikali ya Awamu ya Saba.



Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango na viongozi mbalimbali wakitazama ngoma wakati Mkutano wa Pili wa Umoja wa Mataifa wa Utalii wa Vyakula Afrika jijini Arusha jana. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais)

# Johari: Urekebu wa sheria ni urithi kwa taifa

Na Lidya Inda

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amesema Toleo la Urekebu wa Sheria la 2023 ni urithi wa kihistoria kwa taifa katika kuchagiza maendeleo.

Johari aliyasema hayo Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma jana alipozungumza katika uzinduzi wa toleo hilo, na kueleza kuwa toleo hilo ni urithi wa kisheria kwa wadau wa sekta ya sheria na wadau wa haki na utawala bora.

"Leo tunazindua si tu toleo la urekebu wa sheria, tunazindua urithi wa kisheria kwa wadau wa sekta ya sheria, wadau wa haki na wadau wa utawala bora, hivyo tuitumie ipasavyo kukuza haki na kuchagiza maendeleo ya taifa letu," alisema Johari.

Alisema tofauti na kazi ya kuandaa Toleo la Urekebu wa Sheria Mwaka 2002, toleo hili limefanikishwa kwa kutumia rasilimali za ndani pekee wakati la 2002 lilifadhiliwa na Benki ya Dunia na wataalamu wengi walifanya kazi hiyo walitoka Afrika Kusini.

"Toleo hili ni zao la kazi ya miaka minne yaani mwaka 2020 hadi 2024 na limefanikishwa kwa kutumia rasilimali za ndani pekee chini ya Serikali ya Awamu ya Sita. Hii ni hatua ya kihistoria kwani tofauti na toleo la mwaka 2002 lililofadhiliwa na Benki ya Dunia, awamu hii serikali yako Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) imedhihirisha uwezo wa ndani kwa vitendo," alieleza Johari.

Rais Samia ndiye aliyezindua toleo hilo la mwaka 2023 jana Ikulu ya Chamwino.

Johari alieleza kuwa kazi ya kufanya urekebu wa sheria hizo imeendeshwa na wataalamu wa ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Serikali, jambo linaloashiria dhamira ya kweli ya kujitegemea na kuwekeza katika mifumo imara ya kisheria kwa maendeleo ya taifa.

Akizitaja faida za urekebu wa sheria, alisema ulilenga kufanya majumuisho ya marekebisho ya sheria mbalimbali yanayofanywa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa kitu kimoja ili kurahisisha upatikanaji, usomaji na utumiaji wake.

"Kazi hii ni kazi ya msingi inayolenga kuhuisha, kuboresha na kurahisisha matumizi ya sheria za nchi yetu, kwa kufanya hivyo tunahakikisha sheria zetu zinabaki kuwa hai zinaendana na wakati na zinaeleweka kwa urahisi kwa wananchi wote," alifafanua.

Alisema toleo hilo la urekebu wa sheria linajumuisha sheria kuu 446 ambazo zimepangwa katika juzuu zipatazo 23, ikiwamo fahirisi na miongozo mbalimbali hizo zipo sheria 171 zilizotungwa kati ya mwaka 2002 na 2023.

Pia, alisema kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Urekebu wa Sheria, baada ya kukamilika kwa kazi ya urekebu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atatoa tamko rasmi litakalotangaza tarehe ambayo toleo la urekebu litaanza kutumika.

"Katika tarehe hiyo toleo hilo litaanza kutumika kama sheria halali na sahihi za nchi na litatambuliwa na mahakama zote na mamlaka nyingine kama nakala sahihi ya sheria zilizofanyiwa urekebu. Katika tamko utakalotoa leo, tunapendekeza kuwa tarehe ya kuanza kutumika kwa toleo hili iwe Julai Mosi, mwaka huu ili kutoa fursa ya usambazaji wa sheria hizo kabla ya tarehe ya kuanza kutumika," alieleza Johari.

# Majaliwa ampongeza Samia kuinua sekta ya sheria

Na Selemani Nzaro

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuinua sekta ya sheria.

Majaliwa amesema programu iliyodhaminiwa na Rais Samia ya Kampeni ya Msaada wa Kisheria inayofanyika nchi nzima, imesaidia Watanzania wenye uhitaji wa msaada wa kisheria wapate msaada huo bila malipo.

Alisema hayo Ikulu ya Dodoma jana wakati akimkaribisha Rais Samia kuzindua Toleo la Sheria Zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023.

Majaliwa alisema kampeni hiyo imefanywa nchi nzima kwa sababu taifa lina haraka kubwa ya wataalamu waliobobea katika sheria, na pia wakasaidia katika kufanikisha urekebu wa sheria kwani miaka 20 iliyopita walitumika wataalamu kutoka Afrika Kusini.

"Urekebu huu ni matokeo ya tashwira iliyoko ndani ya nchi kwa uwekezaji mkubwa wa sekta ya sheria katika Serikali ya Awamu ya Sita uliofanywa wewe mheshimiwa Rais," alisema Majaliwa.

Aliongeza kuwa, Rais Samia ana dhamira kubwa ya kufanya maboresho ya sheria katika sekta mbalimbali nchini na Watanzania wanaona na wanajua dhamira yake ya kutaka kuliona taifa linajitegemea kisheria na katika sekta zingine.

Alisema urekebu wa sheria ni mchakato uliofanywa na wataalamu wa ndani ya nchi, hivyo ni vyema Watanzania wakajivunia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Samia katika sekta hiyo.

"Moja ya mambo ambalo tunajua umeweka ngwea kubwa ni kutatatisha sekta ya sheria kwa kuwaelimisha Watanzania ili wasome kuandika jamii iweze kujitambua na kufahamu haki zao za msingi na kupata usimamizi wa kina kwa wote wenye uhitaji wa kisheria," alisema Majaliwa.

# RAIS SAMIA ASAINI TAMKO LA TOLEO LA SHERIA ZILIZOFANYIWA UREKEBU



Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia viongozi pamoja na wageni mbalimbali baada ya kusaini toleo la Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana.



Rais Samia akiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Hamis Juma pamoja na Mwakilishi wa Spika wa Bunge ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dk Joseph Mhagama baada ya kuwakabidhi nakala tatu za Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu.



Matukio mbalimbali wakati wa uzinduzi wa toleo la Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023.



Wageni mbalimbali wakiwa kwenye uzinduzi wa toleo la Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023.



Rais Samia akimkabidhi Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Hamis Juma nakala ya toleo la Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023.




Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari akizungumza kwenye hafla ya kusaini toleo la Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023. (Picha zote na Ikulu).



oagtanzania www.oag.go.tz

majira
GAZETI HURU LA KILA SIKU
www.timesmajira.co.tz
ISSN 0856-5831 ■ NA. 2006 VOL. II/2007
Alhamisi • 24 • MACHI • 2025
BEI: TSHS 1000/KSHS 60

**Woga kikwazo cha mapambano ya VVU Zanzibar**
Uk. 9

**Rais Samia ashiriki Mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi** Uk. 4

**Mwigulu ateta na Mtendaji wa Uendeshaji wa WB** Uk. 3

**Viongozi duniani kushiriki mazishi ya Papa Francis** Uk. 19



# Samia afunguka kuhusu mabadiliko ya sheria

Asema kuanzia mwaka 2002 hadi 2023 marekebisho 1,039 ya sheria mbalimbali yamefanyika, asisitiza jinsi nchi mahitaji sheria zinazokwenda na mabadiliko Uk. 4

**Rais apongezwa mageuzi sekta ya madini**

# Samia afunguka kuhusu mabadiliko ya sheria

**Na Penina Malundo**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kadiri nchi inavyofunguka na kuendelea, ndivyo inavyohitaji mabadiliko ya sheria ili kulinda maslahi ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Pia amesema uzinduzi wa toleo jipya la juzuu za sheria zilizofanyiwa marekebisho ni hatua muhimu katika kupambana na matumizi mabaya ya madaraka na kuongeza uwazi katika utawala wa sheria nchini.

Akizungumza jana Ikulu jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa sheria hizo, Rais Samia alisema kuwa kuanzia mwaka 2002 hadi 2023 jumla ya marekebisho 1,039 ya sheria mbalimbali yamefanyika.

Alisema idadi hiyo inaonesha jinsi nchi inavyofunguka na hivyo kuhitaji sheria zinazokwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Rais Samia alisema kuwa uhuishaji wa sheria haupaswi kuwa tukio la kila baada ya miongo miwili bali kila baada ya miaka 10.

Aidha, ameeleza kuwa ndani ya kipindi hicho cha miaka 10, sheria zinapobadilika zinapaswa kuandikwa na kuingizwa katika mpango wa marekebisho ya kila mwaka, na baadaye kuunganishwa kutengeneza juzuu.

"Serikali itaendelea kuwekeza katika urekebishaji wa sheria ili ziendane na mahitaji ya wakati ambapo urekebu mwingine wa sheria umepangwa kufanyika mwaka 2033.

"Sheria hizo zilizoboreshwa zitaziba mianya ya kisheria ambayo hapo awali ilitumiwa na baadhi ya watu kwa manufaa binafsi, ikiwa ni pamoja na kuchochea vitendo vya rushwa,"alisema.

Aidha, alisema uzinduzi wa toleo jipya la juzuu za sheria zilizofanyiwa marekebisho ni hatua muhimu katika kupambana na matumizi mabaya ya madaraka na kuongeza uwazi katika utawala wa sheria nchini.

"Ile 'tazama kule, tazama kule' ya kisheria ili mtu apenyeze yake saa hakuna. Sheria zimeandikwa upya, zimepangwa vizuri, ziko wazi, zinapatikana kwa urahisi na zinaeleweka kwa wananchi.

Hii itapunguza uwezekano wa watu kutenda makosa kwa kisingizio cha kutojua sheria," alisema Rais Samia.

Alisema kuwa msingi mkuu wa Serikali ni sheria, na bila sheria, hakuna kinachoitwa Serikali.

Rais Samia alinukuu kauli ya Baba wa Taifa "Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliyesema, Serikali ni sheria. Hakuna Serikali bila sheria. Na sheria zikishaundwa, ni lazima zifuatwe," alisema Rais Samia.

Alisema sheria zilizofanyiwa marekebisho si tu nyenzo ya kupambana na rushwa na matumizi mabaya ya madaraka, bali ni msingi imara wa kujenga Taifa linalozingatia haki, amani na maendeleo.

"Waheshimiwa viongozi na wananchi wenzangu, ninapoelekea kuhitimisha niseme kuwa toleo la sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebishaji ni dhamira ya dhati ya Serikali kujenga Taifa linalosimamia utawala bora na wa sheria kwa kuwa na sheria zilizowekwa wazi, zilizo sahihi na zinazoeleweka," amesema Rais Samia.

Toleo hilo la sheria zilizorekebishwa litaanza kutumika rasmi kuanzia Julai 1, 2025, na linatajwa kuwa hatua muhimu katika mageuzi ya kisheria yanayoendelea nchini.

Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hamza Johari alimshukuru Rais Samia kwa kuwezesha kutekelezeka kwa mradi wa Urekebu wa sheria Toleo la mwaka 2023.

Alisema kuwa hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa mradi huo kufanyika kwa rasilimali za ndani ya nchi zikiwemo fedha za makusanyo ya ndani na wataalamu.

Alisema jambo hilo ni hatua ya kihistoria iliyofanikishwa chini ya Serikali ya awamu ya sita, kwani ni tofauti na Toleo la mwaka 2002 ambalo lilifadhiliwa na Benki ya Dunia na kwamba hiyo inaashiria dhamira ya kweli ya Taifa la Tanzania kujitegemea na kuwekeza katika mifumo imara ya kisheria kwa maendeleo ya Taifa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliongeza kuwa urekebu uliofanyika ni kazi ya msingi ambayo inakwenda kuhuisha, kuboresha na kurahisisha matumizi ya sheria za nchi na kwamba kwa kufanya hivyo kutahakikisha kuwa sheria za nchi zitabaki kuwa hai, zinazoendana na wakati na kueleweka na wananchi wote.

Toleo la urekebu lililozinduliwa jana linajumuisha sheria kuu 446 ambazo zimegawanywa katika Juzuu 21 ikiwemo faharasi, ambapo miongoni mwa hizo ni pamoja na sheria mpya 171 zilizotungwa kati ya mwaka 2003 hadi 2023.



oagtanzania
www.oag.go.tz

## Wasira: Viongozi wa dini wametutia nguvu kuendelea na Uchaguzi Mkuu

>>Habari Uk.2



## Mapya yaibuka bungeni sakata tuhuma za Gambo

>>Habari Uk.5

UHURU
ISSN 0876 - 3896 Na. 25229 Alhamisi Aprili 24, 2025 Tanzania sh 1,000
Ukweli Daima



KUELEKEA UCHAGUZI MKUU

"KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE"

@uhuruonline

**446>>**Idadi ya sheria zilizohusishwa katika mabadiliko yaliyofanyiwa urekebu

# Rais Dk. Samia ataja manufaa sheria zilizofanyiwa urekebu



## Rais Dk. Samia ataja manufaa sheria zilizofanyiwa urekebu

Na MUSSA YUSUPH, Dodoma

**446>>Idadi ya sheria zilizohusishwa katika mabadiliko yaliyofanyiwa urekebu**

UZINDUZI



## Wasira: Viongozi wa dini wametutia nguvu kuendelea na uchaguzi mkuu

Na MWANDISHI WETU, Dodoma



oagtanzania
www.oag.go.tz

UWAJIBIKAJI

# Rais Samia: Bila sheria za wazi, haki haiwezi kupatikana

Elizabeth Edward na Sute Kamwelwe, Mwananchi

**Dar es Salaam.** Rais Samia Suluhu Hassan amesema upatikanaji wa haki unatokana na sheria zilizo wazi, zinazofahamika na zinazoendana na wakati tulionao.

Alisema sheria ni kiini cha ustaarabu wa Taifa, bila sheria zilizoandikwa wazi, zinazofahamika na zinazoendana na wakati tulionao, basi haki haiwezi kupatikana.

Akinukuu maneno ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliyewahi kusema kuwa Serikali ni sheria, Rais Samia alisema hakuna kitu kinaitwa Serikali bila sheria na sheria zikishaandikwa ni lazima zifuatwe na zitekelezwe.

Akizungumza jana jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa toleo hilo jipya la juzuu za sheria zitakazoanza kutumika Julai mosi, 2025, Rais Samia alisema marekebisho hayo yanalenga kuendeleza misingi ya utawala bora na utawala wa sheria nchini, ikiwa ni sehemu ya jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha utoaji wa haki.

Alisema tukio hilo ni matokeo ya kazi kubwa na ya kitaalamu iliyofanywa kwa juhudi, weledi na mshikamano wa timu za kisheria zikiongozwa na ofisi ya mwandishi mkuu wa sheria chini ya ofisi ya mwanasheria mkuu wa Serikali.

"Si hivyo tu, bila sheria kuwa wazi hata uhakika wa ulinzi wa haki za raia unatoweka au unakuwa hauna uhakika na kusababisha uvunjifu wa amani, aidha shughuli za uchumi kufanyika kwa mashaka pasipokuwa na sheria za kueleweka," alisema.

"Hata mwekezaji akija, cha kwanza anauliza sheria zetu zinasemaje, sasa kama zipo vipandevipande watakuwa na mashaka, watakosa imani.

"Nyote mnafahamu sheria ni kiini cha ustaarabu wa Taifa, bila sheria zinazofahamika, zilizoandikwa wazi na zinazoendana na wakati haki haiwezi kupatikana," alisema.

Rais Samia alisema bila sheria kuwa wazi uhakika wa ulinzi wa haki za raia unatoweka au unakuwa hauna uhakika na kusababisha uvunjifu wa amani, pia shughuli za kiuchumi kufanyika kwa shaka pasipokuwa na sheria zinazoeleweka.

"Mwekezaji akija anataka kujua sheria zetu zinasemaje, sasa kama ziko vipandevipande anapata shaka na anaweza kukosa imani. Kukamilika kwa toleo hili ni hatua muhimu katika ustawi wa maendeleo ya Taifa," alisema.

Hii ni mara ya pili katika historia ya Tanzania kufanya urekebu wa sheria, shughuli kama hiyo ilifanyika mwaka 2002 na ilihusisha marekebisho ya sheria 415 na toleo hilo jipya linahusisha marekebisho ya sheria 446.

"Serikali ilikuwa ikitoa fedha kwa ajili ya urekebu wa sheria, tukiwa tunafahamu ni kiasi gani, ila leo ndiyo tumejua Sh30 bilioni zimetumika kwenye urekebu wa sheria. Tunajivunia zaidi kwa sababu kazi hii imefanywa na wataalamu wa ndani na sheria hizi zimechapwa na mchapishaji wa hapa nchini, Mkuki na Nyota; safari hii kila kitu kimefanyika hapa nchini na hii ni fahari kwetu," alisema.

Rais Samia alisema uandishi wa juzuu za sheria ni jambo muhimu litakalorahisisha kazi siyo tu kwa wanasheria, mawakili, mahakimu na majaji, bali hata wanaotumia sheria katika utekelezaji wa kazi zao.

"Toleo hili linakwenda kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wananchi na sheria zote kwa 446 zimehuishwa kwenye mabadiliko haya. Sasa hakuna haja kwa wanasheria kuambizana kurejea vifungu vya sheria zilizofanyiwa mabadiliko, sasa sheria zote zimeandikwa upya zipo pamoja katika mpangilio mzuri," alisema.

> **"Si hivyo tu, bila ya sheria kuwa wazi hata uhakika wa ulinzi wa haki za raia unatoweka au unakuwa hauna uhakika na kusababisha uvunjifu wa amani, aidha shughuli za uchumi kufanyika kwa mashaka pasipokuwa na sheria za kueleweka."**
>
> Rais Samia

Kwa upande wa Mahakama, alisema matarajio ni kuwa toleo hilo jipya la sheria litapunguza muda unaotumika kwenye kufanya utafiti ili kupata uhakika wa sheria inavyosema, hivyo kuimarisha utoaji wa uamuzi.

"Pia, juzuu hizi za sheria zilizorekebishwa ni muhimu katika kuongeza uwazi na kusaidia kujenga imani ya wananchi kwa Serikali yao. "Aidha, ni nyenzo muhimu itakayosaidia kupunguza matumizi mabaya ya madaraka na kuziba ombwe la kisheria lililokuwa likitumika kuchochea rushwa," alisema Rais Samia.

"Vilevile kuwekwa vyema kwa sheria hizi kutaongeza mazingira mazuri ya kujenga imani kwa wafanyabiashara na wawekezaji katika kuimarisha shughuli za kiuchumi nchini.



Rais Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Juma nakala ya Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria ya Urekebu wa Sheria katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **Picha na Ikulu**

"Sheria hizi zikipatikana kwa urahisi na zikifahamika vyema kwa wananchi zitapunguza uwezekano kutokea makosa kwa kisingizio cha kutojua sheria."

## Sheria zitaendelea kurekebishwa

Kiongozi huyo mkuu wa nchi alisema Serikali itaendelea kuwekeza kwenye marekebisho ya sheria kuendana na mahitaji yanayojitokeza.

Akimkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Hamza Johari kuwa urekebu wa sheria unapaswa kufanyika ndani ya miaka 20 na kadiri mabadiliko ya sheria yanavyofanyika, ni muhimu kuandikwa upya na kuwekwa kwenye marekebisho ya kila mwaka.

"Nikiangalia takwimu za mwenendo wa kazi wa kutunga na kurekebisha sheria nchini, nimeona katika zoezi la urekebu wa sheria mwaka 2002 idadi ya sheria zilizofanyiwa urekebu zilikuwa 415, mwaka 2023 zimeongezeka kidogo na kufikia 446.

"Hata hivyo, ili kupata picha kamili inabidi kuangalia takwimu za sheria mpya zilizotungwa, zilizofutwa na zilizotungwa upya kuanzia mwaka 2002 hadi 2023. Takwimu hizo zinaonyesha sheria 171 zilifanyiwa mabadiliko makubwa kati ya sheria 446," alisema Rais Samia.

"Pia, takwimu za mabadiliko ya sheria kati ya mwaka 2002 hadi 2023 tunaona jumla ya marekebisho 1,039 yalifanyika kwenye sheria mbalimbali, hii ni kuonyesha kwamba jinsi nchi yetu inavyobadilika na kuleta maendeleo, kunahitajika pia mabadiliko ya sheria zetu ili kufikia utawala bora na haki na maslahi ya jamii na Taifa kwa jumla."

## Alichokisema AG

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa toleo hilo, Johari alisema wakati wa utekelezaji wa mradi huo wa urekebu walikuwa hawafiki ya maboresho yanahitaji kufanyika kwa ajili ya marekebisho ya sheria ya Bunge.

"Wizara ya Katiba na Sheria ilipokea maombi kwa ajili ya kutungwa kwa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali yaliyotokana na zoezi la urekebu. Niishukuru sana wizara kwa kufanikisha hili, [illegible] lilituwezesha kuendelea na utekelezaji wa mradi," alisema.

Johari alisema mradi wa urekebu wa sheria umelenga kufanya maboresho ya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazofanywa na Bunge la Tanzania kuwa kitu kimoja ili kurahisisha upatikanaji na usomwaji wa sheria hizo na ufumbuzi wake.

"Hii ni kazi ya msingi inayolenga kuhuisha, kuboresha na kurahisisha matumizi ya sheria za nchi yetu, kwa kufanya hivi tunahakikisha sheria zetu zinabaki kuwa hai, zinaendana na wakati na zinaeleweka kwa urahisi kwa wananchi wote, zoezi hili linahusisha sheria zote kwa kujumuisha marekebisho yaliyofanyika tangu toleo la mwisho mwaka 2002," alisema Johari.

**Kama una maoni kuhusu habari hii, tuandikie ujumbe kupitia WhatsApp 0765864917**

LUTHERAN WORLD RELIEF

JOB VACANCY

# Samia: Kila sheria itafumuliwa itakapobidi

HABARI UK. 2



Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhi moja ya nakala tatu za sheria za Tanzania kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa ajili ya kumbukumbu, wakati wa hafla ya uzinduzi wa toleo la sheria zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023, Ikulu, Chamwino, mkoani Dodoma jana. Kushoto ni Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma na Mwakilishi wa Spika wa Bunge, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dk. Joseph Mhagama. **PICHA: IKULU**

## Samia: Kila sheria nchini itafumuliwa itakapobidi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassani amesema serikali itaendelea kuwekeza kwenye marekebisho ya sheria za nchi ili kuendana na mahitaji yanayojitokeza.

Alisema hayo jana Ikulu ya Chamwino mkoani hapa wakati akizindua toleo la sheria zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023.

Rais Samia alisema serikali itaendelea kuwezesha marekebisho ya sheria zote za nchi ambazo zitaonekana zinahitaji marebisho kwa mujibu wa mahitaji yanayojitokeza kila wakati, ili kutoa haki kwa kila mtu.

Pia alisema urekebu wa sheria mbalimbali za nchi haupaswi kufanyika kila baada ya miongo miwili kama ilivyo sasa, bali ufanyike kila yanapofanyika marekebisho mapya.

"Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, uhuwishaji sheria zetu haupaswi kusubiri baada ya miongo miwili kama tunavyofanya sasa, bali kila inapofanyiwa marekebisho sheria basi iandikwe upya na kuweka kwenye toleo la kila mwaka na baada ya miaka 10 itangazwe kwenye juzuu," alisema Rais Samia.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kupunguza vitendo vya rushwa pamoja na watu kutumia vibaya madaraka yao kwenye vyombo vya utoaji haki.

"Hili toleo tulilozindua leo (jana) linajumuisha sheria kuu 446 ambazo zimeandikwa upya na kupangiliwa vizuri, hivyo kila mtu anaweza kuzipata na kupunguza watu ambao wamekuwa wanatumia mianya ya marekebisho ya vifungu ambavyo haviingizwa katika sheria kuwanyima haki wengine, ambalo limekuwa linachangia vitendo vya rushwa katika taasisi za haki jinai nchini," alisema.

Rais Samia pia alimwagiza Mwandishi Mkuu wa Sheria kuharakisha mchakato wa kufanya tafsiri ya sheria hizo zilizoandikwa upya kwa Kiswahili ili wadau wa sheria pamoja na wananchi waweze kunufaika nazo.

"Agizo langu kwako Mwandishi Mkuu wa Sheria ni kuhakikisha unazifanyia tafsiri sheria hizi zote kwa lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo inatumika ili wadau wa sheria pamoja na wananchi wanufaike nazo na kusaidia kupunguza migogoro katika jamii zetu," alisema Rais Samia.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, alisema toleo hilo la sheria zilizofanyiwa urekebu limetoka ikiwa ni baada ya miaka 23 kupita.

Johari alisema, "Mheshimiwa Rais, toleo la mwisho kutoka kabla ya leo (jana) lilikuwa ni mwaka 2002, liliwezeshwa na Benki ya Dunia (WB), lakini hili la mwaka huu ni fedha za serikali na wataalamu wote walioitumika pamoja na mchapishaji ni kutoka ndani ya nchi."

# Dkt. Samia aagiza kukamilishwa zoezi la kutafsiri Sheria za TZ kwa Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

RAIS Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiagiza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukamilisha zoezi la kutafsiri Sheria za Tanzania kwa lugha ya Kiswahili ikiwemo Toleo la Sheria za Tanzania la Mwaka 2023.

Aliagiza kuwekwa utaratibu utakaowezesha kupatikana kwa nakala za Toleo la Sheria zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023 ikiwemo kutumia TEHAMA ili wananchi wazipate kwa urahisi kwenye mitandao kwa minajili ya kujifunza na kujua haki zao.

Rais Dkt. Samia alitoa agizo hilo jana katika uzinduzi wa Toleo la Sheria za Tanzania zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023 hafla iliyofanyika Ikulu ya Chamwino.

"Sheria ni kioo cha ustaarabu wa Taifa, bila sheria zilizowekwa wazi haki haiwezi kupatikana, bila sheria kuwa wazi uhakika wa ulinzi wa haki ya raia unatoweka, kusababisha uvunjifu wa amani na shughuli za kiuchumi zinafanyika kwa mashaka," alisema Rais Dkt. Samia.

Alieleza kuwa, kutokuwepo Juzuu za Sheria zilizorekebishwa kwa wakati huchangia wananchi kunyimwa haki zao kwa sababu wanaotumia kutoloa maamuzi hawana uelewa wa uwepo wa sheria mpya.

"Kukamilika kwa Toleo la Sheria zilizofanyiwa Urekebu kutarahisisha upatikanaji haki kwa wananchi kwa kuwa Sheria zote kuu 446 zimehuishwa, zinapatikana kwa pamoja na kwa urahisi, zimepangwa vizuri.

"Pia upatikanaji wa toleo lililozinduliwa utasaidia kupunguza muda wa Mahakama kufanya utafiti kabla ya kufanya maamuzi, kuongeza uwazi na kuwajengea wananchi imani kwa Serikali.

"Kupunguza matumizi mabaya ya madaraka kwa kuziba ombwe la kisheria linalochochea mianya ya rushwa, kuimarisha utawala wa sheria, kuongeza hadhi ya nchi kiuchumi, kisiasa na kijamii," alisema.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia aliagiza zoezi la Urekebu wa Sheria lifanyike kila baada ya miaka 10 badala ya sasa ambapo limefanyika baada ya miaka 20 tangu zoezi kama hilo kufanyika miaka 23 iliyopita mwaka 2002.

Pamoja na hayo, Rais Dkt. Samia amebainisha kuwa mbali ya kusubiri zoezi hilo la miaka 10, kila mara Sheria zinaporekebishwa, marekebisho hayo yajumuishwe kila mwaka na yapatikane kidijiti kwa kutumia TEHAMA.

Uzinduzi wa Toleo la Sheria za Tanzania zilizofanyiwa Urekebu Mwaka 2023 unadhihirisha dhamira ya Serikali kujenga Taifa linalosimamia utawala wa sheria, kuwa na sheria zilizowekwa wazi, zilizo sahihi, zinazoeleweka.



# Dk. Samia: Marekebisho ya sheria kurahisisha upatikanaji haki

NA MWANAJUMA ABDI

**RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema toleo la sheria zilizofanyiwa marekebisho (urekebu) la mwaka 2023, litasaidia kurahisisha upatikanaji wa haki katika jamii, sambamba na wananchi kuongeza imani kwa serikali.**

Dk. Samia ameyaeleza hayo jana Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma kwenye hafla ya uzinduzi wa toleo la sheria zilizofanyiwa marekebisho ya mwaka 2023, iliyokwenda sambamba na utiaji saini ili kuanza kutumika rasmi kwa sheria hizo.

Alisema sheria hizo zilizofanyiwa marekebisho zitawasaidia watu maarufu wa kisheria na kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wananchi, ambapo kazi cha sheria 446 zimehuishwa katika mabadiliko hayo.

Dk. Samia alieleza kuwa tukio la utiaji saini na kuanza kutumika kwa sheria hizo ni la kihistoria, ambapo ni miongoni mwa hatua zinazochukuliwa na serikali katika kuimarisha utawala wa sheria.

"Tuna sheria zilizoandikwa upya na sasa hakuna haja kwa wanasheria kuambizana 'hebu refer' sheria ya mwaka gani, hebu 'refer' kifungu cha sheria cha mwaka fulani. Sheria zimeandikwa upya na zinapatikana pahali pamoja na kufanyakazi kuwa rahisi", alisema.

Alisema hatua hiyo imerahisisha mahakama kwenda sambamba na sheria inavyotaka na kurahisisha maamuzi, hivyo marekebisho hayo ni muhimu katika kuongeza uwazi na upatikanaji haki.

Alibainisha kuwa sheria hizo zikipatikana kwa urahisi na zikifahamika vyema na wananchi zitapunguza uwezekano wa kufanya makosa kwa kisingizio cha kutokujua sheria, hivyo kwa ujumla zoezi hilo la urekebu limejibu zile changamoto za msingi kwenye tasnia ya sheria.

Hata hivyo, alisema takwimu za sheria mpya zilizotungwa, zilizofutwa na kutungwa upya kuanzia mwaka 2002 hadi mwaka 2023, takwimu hizo zinaonesha kwamba sheria 171 zilifanyiwa mabadiliko makubwa kati ya sheria 446.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alimpongeza Dk. Samia kwa kueleza kuwa zoezi hilo lilikuwa likitekelezwa huko nyuma kwa kutumia fedha kutoka taasisi za kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, lakini hivi sasa limefanyika kwa kutumia fedha za ndani na wataalamu wazalendo.

Majaliwa alisema Dk. Samia ameongeza uwekezaji katika elimu na taaluma mbalimbali katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita, ikiwemo kuimarisha sekta ya sheria kwa kuwaelimisha watanzania ili jamii iweze kujitambua, kufahamu haki zao za msingi.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari alisema toleo la urekebu la sheria la mwaka 2023 ni urithi wa kisheria wa taifa, hivyo litumike ipasavyo katika kukuza haki na kuchagiza maendeleo ya taifa.



*RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan akisaini nakala za sheria za Tanzania zilizofanyiwa marekebisho (urekebu) kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha sheria ya urekebu wa sheria, hafla hiyo ilifanyika Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma. (PICHA NA IKULU).*

## Dk. Khalid aitaka bodi ZAA kufikia malengo

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, amesema mashirikiano katika utendaji ni miongoni mwa njia muhimu zitakazoleta mafanikio na kufikiwa kwa malengo na ufanisi mkubwa.**

Dk. Khalid ameleza hayo jana wakati akifungua bodi ya tano ya wakurugenzi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa jengo la uwanja wa kimataifa wa Abeid Amani Karume (ZAA).


Amesema yakiwepo mashirikiano katika utendaji baina ya uongozi na





*RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, nakala za sheria za Tanzania zilizofanyiwa marekebisho kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha sheria ya urekebu kwa ajili ya kumbukumbu, hafla iliofanyika Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma. (PICHA NA IKULU).*

# Rais Samia atoa muongozo marekebisho ya sheria



**MSOFE: WAZAZI CCM ILALA YAUNGANA NA WAKOTOLIKI KUOMBOLEZA KIFO CHA PAPA**

SOMA UK.2



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ashiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi kuhusu mabadiliko ya Tabianchi kuelekea Mkutano wa COP30 kwa njia ya Mtandao, Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma

- Aagiza zoezi la urekebishaji sheria lifanyike kila baada ya miaka 10 badala ya miaka 20
- Asema mbali ya kusubiri zoezi hilo la miaka 10, marekebisho hayo yajumuishwe kila mwaka

SOMA UK.2

# Majaliwa: Mama Samia Legal Aid ni suluhisho

- Asema imekuwa jibu la mafumbo mengi katika changamoto za kisheria kwa wanyonge wengi
- Sasa imekuwa kimbilio la wananchi kwenye kutatuliwa migogoro mbalimbali
- Ampongeza Rais Dkt. Samia kwa kuendelea kuimarisha na kuwekeza kwenye sekta ya sheria nchini

>>SOMA UK.4

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaini nakala tatu za Sheria za Tanzania zilizofanyiwa urekebu kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria ya urekebu wa sheria, Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma jana. Picha na Ikulu



**Mdee atuma kombora kwa Mrema uchambuzi wake wa sheria, kanuni za uchaguzi**

>>SOMA UK.2





oagtanzania
www.oag.go.tz



Hakimu. Umoja. Amani. Ni nguzo Zetu!

NCHI YETU

Tanzania imara, Kazi Iendelee

www.maelezo.go.tz | Toleo Na. 894 | Aprili 23, 2025 | Idara ya Habari MAELEZO | TANZANIA

# Rais Azindua Toleo la Sheria Zilizofanyiwa Urekebu

# Sheria Zilizofanyiwa Urekebu Kurahisisha Upatikanaji wa Haki

Na Jacqueline Mrisho, MAELEZO


RAIS DKT. SAMIA: MRADI WA UREKEBISHAJI SHERIA NI HATUA MUHIMU KWA MAENDELEO YA TAIFA
/fullshangweblog

oagtanzania



View insights

Boost post

48 3 2

Liked by **leilamuhaji** and others

**oagtanzania** HABARI PICHA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 23 Aprili, 2025 ametia Saini tamko la  Sheria Kuu  446 za Tanzania zililofanyiwa Urekebu toleo la Mwaka 2023.

oagtanzania




View insights

Boost post

29 2 1

Liked by **leilamuhaji** and others

**oagtanzania** USIKOSE KUFUATILIA TAARIFA MUHIMU KUTOKA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI, LEO TAREHE 23 APRILI, 2025.

BONGO5 HABARI BURUDANI MICHEZO VIDEOS Log In

# Ofisi ya AG yapendekeza Julai Mosi kuanza kutumika kwa toleo la sheria zilizofanyiwa urekebu

Yasini Ngitu · 2 days ago · 2 minutes read

Facebook X



Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Hamza Johari amesema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imependekeza Julai Mosi, 2025 iwe ni tarehe ya kuanza kutumika kwa toleo la sheria zilizofanyiwa urekebu la mwaka2023.

Johari ameyasema hayo leo Aprili 23, 2025 wakati wa hafla ya uzinduzi wa Toleo la Sheria zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023 iliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Amesema pendekezo la tarehe hiyo ni ili kutoa fursa ya usambazaji wa sheria hizo kabla ya tarehe ya kuanza kutumika na kwamba ameeleza kuwa baada ya tarehe hiyo toleo hilo litaanza kutumika kama sheria halali na sahihi za nchi na litatambuliwa na mahakama zote na mamlaka zingine kama rejea sahihi ya sheria zilizofanyiwa urekebu.

Hata hivyo Johari amesema urekebu wa sheria ni mradi walioufanya uliolengo kufanya majumuisho ya marekebisho ya sheria mbalimbali yanayofanywa na Bunge kuwa kitu kimoja ili kurahisisha upatikanaji, usomwaji na utumiaji wa sheria hizo.




# Awamu ya Sita Yafanikisha Urekebu wa Sheria kwa Rasilimali za Ndani


**Na Jacqulline Mrisho, MAELEZO**

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanikisha zoezi la uandishi wa Sheria zilizofanyiwa urekebu la Mwaka 2023, kwa kutumia wataalam wazawa na kampuni ya wachapishaji wazawa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Saidi Johari amesema hayo leo Aprili 23, 2025 Ikulu, Chamwino jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa Toleo la Urekebu wa Sheria la Mwaka 2023 uliofanywa na Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mhe. Johari amesema kuwa, kumekuwa na mageuzi na jitihada mbalimbali katika usimamizi wa sheria na katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo kwa namna moja ama nyingine yamechagiza kukamilika kwa zoezi la urekebu wa sheria ambapo mageuzi hayo yanajumuisha kuongeza nguvu kazi kwa kuajiri zaidi ya Mawakili wa Serikali 50 na kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

"Utekelezaji huu ni zao la kazi ya miaka minne chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ambapo limefanikishwa kwa kutumia rasilimali za ndani pekee. Hii ni hatua ya kihistoria, kwani ni tofauti na Toleo la mwaka 2002 ambalo lilifadhiliwa na Benki ya Dunia. Awamu hii, Serikali yako imedhihirisha uwezo wa ndani kwa vitendo na hivyo kuashiria dhamira ya kweli ya kujitegemea na kuwekeza katika mifumo imara ya kisheria kwa maendeleo ya Taifa letu", amesema Mhe. Johari.





Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanikisha zoezi la uandishi wa Sheria zilizofanyiwa urekebu la Mwaka 2023, kwa kutumia wataalam wazawa na kampuni ya wachapishaji wazawa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Saidi Johari amesema hayo leo Aprili 23, 2025 Ikulu, Chamwino jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa Toleo la Urekebu wa Sheria la Mwaka 2023 uliofanywa na Rais, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan.

Mhe. Johari amesema kuwa, kumekuwa na mageuzi na jitihada mbalimbali katika usimamizi wa sheria na katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo kwa namna moja ama nyingine yamechagiza kukamilika kwa zoezi la urekebu wa sheria ambapo mageuzi hayo yanajumuisha kuongeza nguvu kazi kwa kuajiri zaidi ya Mawakili wa Serikali 50 na kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

"Utekelezaji huu ni zao la kazi ya miaka minne chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ambapo limefanikishwa kwa kutumia rasilimali za ndani pekee. Hii ni hatua ya kihistoria, kwani ni tofauti na Toleo la mwaka 2002 ambalo lilifadhiliwa na Benki ya Dunia. Awamu hii, Serikali yako imedhihirisha uwezo wa ndani kwa vitendo na hivyo kuashiria dhamira ya kweli ya kujitegemea na kuwekeza katika mifumo imara ya kisheria kwa maendeleo ya Taifa letu", amesema Mhe. Johari.




habariclouds and cloudstv




340 5

**habariclouds** Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hamza Johari amesema kuwa zoezi la Urekebu wa Sheria litafanyika kila baada ya miaka 10 kama Sheria inavyohitaji na hii inatokana na uwekezaji wa teknolojia ya rasilimali watu.


DIGITAL
Aprili 24, 2025
HABARI
TANZANIA YAWEKA HISTORIA
GHARAMA ZA UREKEBU WA SHERIA
ITVTanzania / itvtz / www.itv.co.tz


TBC Digital
TBC Digital
Jambo TANZANIA
Fahamu kuhusu Urekebu wa Sheria
@tbc_online
tbcdigital@tbc.go.tz
#Usipitwe

oagtanzania



View insights

Boost post

35

Liked by **officialtcaa** and others

**oagtanzania** *OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI YAKAMILISHA MRADI WA UREKEBU WA SHERIA NCHINI.*

# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora